JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Namba ya mkuu wa shule **0784944532/0714863623**

Makamu mkuu wa Shule **0784644315**

Patron **0687068528/0718218647**

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……
……
S. L. P…….
……

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI HALMASHAURI YA LUSHOTO MKOA WA TANGA MWAKA 2018**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule ya Sekondari ya **Shambalai** Mwaka **2018.** Shule hii ni ya Bweni yenye tahasusi ya **HGL na HKL**. Shule ipo umbali wa **Kilometa 2** kutokea stendi ya mabasi **Lushoto**. Usafri wa kutoka mjini Lushoto ni gari ndogo maarufu **VIDOCHI** nauli ni shilingi **500/=** au usafiri wa pikipiki (bodaboda) ni shilingi **1000/=**
   Muhula wa masomo unaanza tarehe **02/07/2018**. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **02/07/2018**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **16/07/2018**.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-
   2.1 Sare ya shule
      a) Sare ya shule ni:
         1. Suruali Nyeusi yenye marinda upana wa chini usiwe chini ya inchi 16
         2. Shati jeupe mikono mirefu
         3. Tracksuit nyeusi
         4. Soksi jozi mbili nyeupe
         5. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
         6. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi
         7. Sweta rangi ya blue

8. Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali nyeusi na T-shirt. T-shirt zinapatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 10,000/= kwa kila moja (Mwanafunzi anaweza kuwa na T-shirt zaidi ya moja). **MAVAZI MENGINE TOFAUTI NA SARE YA SHULE NA SHAMBA DRESS HAYARUHUSIWI.**
9. Tai nyeusi yenye mistari myeupe

**2.2 Ada na Michango ya Shule**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi elfu sabini (70,000/=) kwa mwanafunzi wa Bweni. Unaweza kulipa shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa maramoja

**b) Michango Inayotakiwa Kulipwa Na Kila Mzazi Ni:-**

i. Shilingi **15,000/=** kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii. Shilingi **6,000/=** kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii. Shilingi **20,000/=** kwa ajili ya taaluma.
iv. Shilingi **30,000/=** kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
v. Shilingi **2,000/=** nembo ya shule.
vi. Shilingi **10,000/=** kwa ajili ya huduma ya kwanza Tshs. 5,000/=, na Bima ya Afya Tshs. **5,000/=** (wanafunzi washauriwe kujiunga na mfuko wa bima ya afya CHF kikaya)
vii. Shilingi **20,000/=** Mitihani ya kujipima (mock)
viii. Shilingi **10,000/=**kukodisha godoro kwa muhula (yanapatikana shuleni)
ix. Fedha ya tahadhari **5,000/=** (haitarejeshwa)
Jumla ya michango ni shilingi **118,000/=**

**ANAGALIZO:** Jumla ya ada na michango kwa mwanafunzi ni shilingi **188,000/=. Mwanafunzi atakaporipoti atatakiwa awe amelipa angalau kiasi cha Shilingi 153,000/= La sivyo hatapokelewa.** Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na. **41601100002 (JINA LA AKAUNTI NI: SHAMBALAI SECONDARY SCHOOL FUND)** Benki ya NMB Lushoto (**Tafadhali Andika Jina La Mwanafunzi Kwenye Pay In Slip na Iwasilishe Shuleni)**

**c) Mahitaji Muhimu Ambayo Mwanafunzi Anapaswa Kuleta Shuleni Ni:-**

i) Ream 1 aina ya A4(kwa mwaka)
ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha iambatanishwe)
iii) Mashuka pair mbili rangi ya blue bahari, blanketi 1, chandarua 1.
iv) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
v) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
vi) Panga/kwanja 1, jembe 1, squezer 1, fagio 1
vii) Result slip (original na nakala)
viii) Picha mbili (Passport size) zilizopigwa na shati jeupe.

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kuwa na nywele ndefu
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix. Uvutaji wa sigara
x. Uasherati,uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kushiriki kupata ujauzito/kutoa mimba
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za Nchi.
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi.
xvi. Kudharau bendera ya taifa
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatanisho Na Fomu Muhimu**

a. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi au mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai na Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo au maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI

……

**MWANGA YONA WETUNDWA**

MKUU WA SHULE

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
**OR-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
**Shule ya Sekondari Shambalai**
**FOMU YA HISTORIA/MKATABA WA MWANAFUNZI**

Ajaze Mwanafunzi
1. Jina Kamili……

2. Tarehe ya Kuzaliwa…….

3. Uraia……

4. Dini…….

5. Shule ya Sekondari uliyosoma……

| Na. | Jina la mwanafunzi | Shule Msingi/Sekondari uliyosoma | mwaka uliomaliza |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

Mimi…….....mwanafunzi wa kidato…….Mkondo……
Mwaka…… Naahidi kutekeleza na kufuata sheria/kanuni na taratibu za shule ya sekondari Shambalai iliyoko Lushoto mjini. Ikitokea nimekiuka taratibu za shule hatua kali za kinidhamu zichukuliwe juu yangu.

Saini ya mwanafunzi…… Tarehe……..

**Maelezo Binafsi ya Mzazi/Mlezi:**
a) Jina la Mzazi/Mlezi …….. saini……
Kazi afanyayo……..….
Anuani …….……. Simu…….

Naahidi kwamba nitamsisitiza mwanangu kufuata sheria/kanuni za Shule ya Sekondari Shambalai. Na pia sitampa simu mwanafunzi anapokuja shuleni kwa kuwa natambua kuwa simu haziruhusiwi kwa mwanafunzi. Hivyo nitashirikiana na Uongozi wa Shule kuhakikisha mwanangu anazingatia makubaliano haya. Kama akishindwa kuzingatia, hatua kali zichukuliwe dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufukuzwa Shule.
Mimi…….. Mzazi/Mlezi wa……....

Saini …… Tarehe……

*The united Republic of Tanzania*
**PO- Regional Administration and Local Government**

Shambalai Secondary School
P.O BOX 52
Lushoto
…….

Ref.No. SSS/C/PS/V.1/12
To the Medical Officer
……,
……..…..,
…….

**Ref: A PUPIL'S MEDICAL EXAMINATIONS FORM**

Please, examine the Pupil…… in respect of these areas and any other area(s) deemed fit Please. Delete whichever applies.
Does the Pupil have problems in connection with……..?
a) Sight Yes/No. If yes, state…….....

……
b) Hearing. Yes/No. If yes, state ……...

……
c) T.B or any other Chronic Diseases. Yes/No. If yes, state ……

……
d) Blood Pressure. Yes/No. If yes, state ……....

……
e) Any Physical Impairment(s). Yes/No. If yes, state ……
……
Do you therefore recommend this pupil to pursue studies at this school?
……
……
…….

Name. ……Signature. …….. Date……

Official Title…….. Official Stamp.